# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

## HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI MHE. PAULINE GEKUL (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2015.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI MHE. PAULINE GEKUL (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji kwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,** pili napenda kuwapongeza viongozi wote wa vyama vinavyounda UKAWA ambavyo ni CUF, NCCR-Mageuzi, NLD na CHADEMA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwaelimisha watanzania umuhimu wa kuwa na mageuzi ya kisiasa katika nchi yetu na hivyo kuwahamasisha kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga kura ambalo linafanyiwa maboresho hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura ili waawe na sifa ya kupiga kura katika uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani

unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2015. *"Ewe mwananchi, Kura yako ni maisha yako!! Jitokeze ukajiandikishe*"

## 2. UWEZESHAJI

### 2.1. Mifuko ya Uwezeshaji

**Mheshimiwa Spika,** ninawasilisha maoni haya nikiwa na masikitiko makubwa kwa kuwa Serikali hii ya awamu ya nne CCM inamaliza muhula wake wa pili wa utawala ikiwa imewaacha watanzania katika lindi la umasikini uliokithiri baada ya kuwahadaa wananchi kuwa ingewawezesha kujikwamua na umasikini. Mfano mzuri wa hadaa kwa wananchi ni pale ambapo Serikali hii ya CCM ilijigamba kwa mbwembwe kuwa inawawezesha wananachi kupitia "Mabilioni ya Kikwete" ambapo programu hiyo iliyeyuka kimyakimya na mpaka sasa haiujulikani ilinufaisha wananchi wangapi na imesaidia kwa kiasi gani kupunguza umasikini kwa watanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kama kweli mfuko huo wa Mabilioni ya Kikwete ulianzishwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi na sio propaganda ya kuwatapeli wananchi, basi ungekuwa endelevu, na uendelevu wake ungetokana na marejesho ya fedha hizo kugawiwa kwa wananchi wengine ili nao wajikwamue kiuchumi. Kwa hiyo fedha hizo zingekuwa ni fedha zinazozunguka (Revolving Fund). Lakini mpaka sasa haijulikani kama fedha hizo zipo au zimeshaliwa na wajanja!!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa mrejesho wa matumizi ya fedha za mabilioni ya kikwete kwa kuzingatia idadi ya wananchi walionufaika na mikopo iliyotokana na fedha hizo na mchango wa fedha hizo katika ukuaji wa uchumi. Wakati huohuo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha hizo kwa kuwa ni fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kwamba kuna mifuko 12 ya uwezeshaji lakini mifuko hiyo haipo katika uratibu na usimamizi madhubuti ndio maana haina tija inayokusudiwa. Mifuko hiyo ni kama ifuatavyo:

i. Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (MEF)
ii. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF)
iii. Small Enterpreneurs Loan Facility (SELF)
iv. National Enterpreneurs Development Fund (NEDF)
v. Agricultural Input Trust Fund (AGITF)
vi. Presidential Trust Fund (PTF)
vii. Rural Energy Fund (REF)
viii. Vodacom Foundation
ix. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF)
x. Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)
xi. Small and Medium Enterprise Guarantee Scheme (SME – CGS)

xii. Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wanawake katika Sekta isiyo rasmi

xiii. Tanzania Sociaol Action Fund (TASAF)

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kuwa na mifuko ya uwezeshaji mingi namna hiii chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa kuna mifuko inayotoa huduma zinazofanana na hizi katika Wizara za kisekta. Kwa mfano hakuna haja ya kuwa na Mfuko wa Rural Energy Fund chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu wakati kuna Mfuko wa fedha za REA chini ya Wizara ya Nishati na Madini kwa ajili ya usambazaji wa umeme vijijijini. Halikadhalika hakuna haja ya kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) wala Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake(WDF) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji wakati kuna Mfuko mwingine TAMISEMI wenye utaratibu wa kutoa asilimia 10% ya Mapato ya ndani ya kila Halmashauri kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake. Isitoshe kuna Benki ya Wanawake chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto nk.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu huu wa kuwa na mifuko inayotoa huduma zinazofanana kuwa chini ya mamlaka tofauti kunawachanganya wananchi juu ya wapi hasa wanatakiwa kupata huduma husika. Aidha, mchanganyiko huu unasababisha matumizi mabaya ya fedha za umma kwani kuna watu wameajiriwa kusimamia mifuko hii na wanalipwa lakini kazi wanazofanya ni zilezile ambazo zingeweza kufanywa na mamlaka moja. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inashauri kwamba, mifuko hii ya uwezeshaji iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo inatoa huduma zinazofanana na mifuko mingine katika Wizara za kisekta, ifutwe na badala yake ibaki ile mifuko katika Wizara za kisekta ili wananchi waweze kupata huduma kwa urahisi zaidi na bila mkanganyiko katika Wizara ya Sekta husika.

## 2.2. Kiini Macho cha Mikopo ya asilimia 5 ya Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa Vijana na Wanawake:

**Mheshimiwa Spika,** ni utaratibu wa kisheria kwamba kila Halmashauri inapaswa kutenga asilimia 5 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha wanawake na vijana. Ila jambo la kushangaza ni kwamba agizo hili la kisheria halitekelezwi ipasavyo. Kwa mujibu wa ripoti ya CAG ya 2012/13 zaidi ya asilimia 90 ya Halmashauri zote nchini hazitengi fedha hizo na zile zinazojitahidi kutenga fedha hizo, zinatenga chini ya kiwango kilichowekwa cha asilimia 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri, lakini mbaya zaidi fedha hizi zimekuwa zikitolewa kwa ubaguzi na wakati mwingine zinatumika kutekeleza malengo ya kisiasa ya Chama cha Mapinduzi na haziwafikii walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia imeshtushwa sana kuona kwamba hata zile Halmashauri ambazo zina wabunge ambao ni mawaziri wa TAMISEMI zimetenga fedha hizo chini ya kiwango na nyingine

hazikutenga kabisa. Kwa mfano Halmashauri ya Mtwara ambapo Waziri Hawa Ghasia anatoka ilitenga asilimia 1.8 tu ya mapato ya ndani kwa ajili ya vijana na wanawake badala ya asilimia 10%. Mfano mwingine ni Halmashauri ya Siha ambako anatoka Naibu Waziri OWM – TAMISEMI. Halmashauri hii hadi kufikia machi, 2015 ilikuwa haijapeleka hata senti moja katika mfuko huu wa vijana na wanawake.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, kama mawaziri hawa wana uhalali wa kuendelea kusimamia wizara hii inayogusa maisha ya watanzania masikini ikiwa wameshindwa hata kutekeleza agizo hili la kisheria katika halmashauri zao kwa vitendo ?

**2.3. Uwezeshaji katika Ajira**

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Rais Jakaya Kikwete alipokuwa akigombea Urais kupitia CCM aliwaahidi watanzania na hasa vijana kuwa angesaidia kupatikana kwa ajira milioni moja. Nasikitika kwamba Rais pia alipokuwa akihutubia katika sherehe za Mei Mosi mwaka huu alijigamba kuwa wamevuka lengo la ajira milioni moja kwa kuwa kwa mika kumi ya utawala wa CCM ajira zimepatikana **2,653,544** ikiwa kati ya hizo ajira **600,547** zilitolewa na sekta ya umma na ajira **2,052,997** zilitokana na sekta binafsi**.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Tanzania ina zaidi ya wananchi milioni 22 wanaostahili kuajiriwa lakini hawana ajira. Ikiwa Rais anajivunia kuwapatia ajira

wananchi milioni mbili tena kwa muda wa miaka kumi aliyokaa madarakani ajue pia kwamba kuna watanzania zaidi ya milioni 20 ambao hawana ajira na idadi hiyo inaongezeka kila mwaka kutokana na wahitimu wa ngazi za elimu ya juu wanaohitimu masomo yao kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la Serikali hii ya CCM ni kufanya propaganda na mzaha kwa masuala muhimu katika Taifa. Na mzaha huu unafanyika kwa kujiwekea malengo kidogo na inapoyatekeleza kwa makadirio hayo madogo, inajitapa kuwa imevuka malengo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta katika Bunge hili Mpango Mkakati wa kukuza ajira nchini na sio kutegemea ahadi hewa za CCM inazofanya katika kampeni za uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** madhaifu haya yote yanayofanywa na Serikali ya CCM yanaturejesha kwenye wosia ya Hayati Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake cha "Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania" uk. 51 wakati akizungumzia jinsi Serikali na chama zilivyoshindwa kushughulikia masuala muhimu ya nchi: Mwalimu alisema "Lakini hatulazimiki kuendelea na uongozi mbovu wa chama na Serikali. Wala tukiendelea na hali hiii bila kubadili uongozi wa chama na Serikali, sina hakika kama tutafika huko salama.

**Mheshimiwa Spika,** wosia huu umekuja wakati muafaka. Kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu, ni vema wananchi wakatambua kwamba huu ndio wakati wa

kukikataa chama na Serikali yake iliyoshindwa kutekeleza mahitaji yao ya msingi kwa miaka 50 ya uhuru.

## 3. UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji ni moja ya nyenzo zinazosaidia kasi ya ukuaji wa uchumi na huduma nyingine za kijamii. Uwekezaji unaweza kufanywa na wawekezaji wazalendo katika uwekezaji wa ndani, na unaweza pia kufanywa na wawekezaji wa kigeni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba masuala ya uwekezaji hapa nchini yanaratibiwa na kuongozwa na sheria ya uwekezaji namba 26 ya mwaka 1997. Hata hivyo, Sheria hiyo imeweka masharti magumu kwa wawekezaji wa ndani jambo linalowafanya wataanzani wengi washindwe kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi. Kwa mfano sheria inamtaka mwekezaji wa ndani kuwa na mtaji usiopungua dola za kimarekani 100,000 sawa na Tsh mil 200 ili aweze kutambulika kama mwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kiwango hicho cha mtaji kinawafanya watanzania wengi washindwe kuwekeza katika nchi yao kwa kuwa hawana fedha hizo. Hata pale ambapo wangekopa katika mabenki, riba ziko juu sana kiasi kwamba mwekezaji huyu hawezi kupata faida  isipokuwa kutumikia mabenki kwa kulipa riba za mkopo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta Bungeni muswada wa marekebisho wa sheria ya uwekezaji nchini ili kurekebisha kipengele kinachohusu kima cha chini cha mtaji kwa kupunguza kima

hicho ili watanzania wengi waweze kuwa na sifa ya kuwa wawekezaji katika nchi yao katika miradi mbalimbali.

### 3.1. Matumizi mabaya ya fedha katika Miradi ya Maendeleo

### 3.1.1. Mradi wa Kukuza Ushindani wa Sekta Binafsi (PSCP) na Road Map ya Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 1 na milioni 40 kwa ajili ya miradi ya maendeleo chini ya wizara hii. Katika fedha hizo shilingi milioni 200 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi milioni 840 zilikuwa ni fedha za nje. Kwa mujibu wa randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu fungu 37( uk. 12) kwa kipindi cha Julai 2014 na machi, 2015 ofisi ilipokea fedha za nje jumla ya shilinig bilioni 2 na milioni 225 sawa na asilimia 265 ya bajeti iliyopangwa awali kwa ajili ya utekelezaji miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** jambo la kushangaza ni kwamba fedha zote zimetumika kama matumizi mengineyo (OC)kwa ajili ya mikutano, warsha na safari. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni kwa nini fedha zote zilitumika kwa matumizi ya kawaida badala ya kutekeleza mradi? Aidha ni kwa nini Serikali ilipeleka fedha nje ya bajeti ya shilini bilioni moja na milioni 40 na badala yake ikapeleka bilioni 2 na milioni 225 na zikatumika zote wakati kuna miradi mingi haipelekewi fedha kama ilivyopangwa katika bajeti?

### 3.1.2. Mwingiliano wa kazi za Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji na Wizara za Kisekta

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali ilivyo sasa wizara hii inasimamia utafutaji wa wawekezaji katika miradi mikubwa inayotekelezwa na wizara za kisekta. Kwa mfano miradi ya bandari, reli, nishati, viwanja vya ndege na barabara kwa sasa inashughulikiwa na wizara hii kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji( uk.6) jambo ambalo lingefanywa na wizara husika ili kuongeza ufanisi na kupunguza urasimu na gharama za uendeshaji wa serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi, ni kwa nini inatoa majukumu yanayofanana kwa wizara mbili tofauti? Je, huu si ufujaji wa fedha za umma kwa kuwalipa watumishi katika wizara mbili tofauti kwa kazi zilezile?

## 4. Kituo cha Uwekezaji ( TIC)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa sheria ya Uwekezaji namba 26 ya 1997, moja ya majukumu ya kituo cha uwekezaji ni kuwasaidia wawekezaji wote ikiwa ni pamoja na wale ambao hawabanwi na sheria hii kupata vibali vyote muhimu, usajili na idhini zinazohitajika katika kumwezesha mtu kuwekeza katika nchi na pia kuwezesha upatikanaji wa hati halali za kituo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali ilivyo sasa, Tanzania imekumbwa na wimbi kubwa la wageni ambao wanaingia nchini kwa

shughuli mbalimbali. Hii inadhihirishwa na Mtiririko wa Mitaji kutoka nje (FDI) Afrika mashariki ambapo kwa ripoti ya 2013 Tanzania inaongoza kwa kupokea mitaji mingi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,872 ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** kambi rasmi ya upinzani inaitaka serikali kueleza ni jinsi gani kituo cha uwekezaji kinaratibu shughuli za wawekezaji hawa kwa kuwa hivi sasa kuna wimbi kubwa la wageni wanaofanya biashara ndogondogo nchini ambazo zingeweza kufanywa na wazawa.

**5. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya 2014/15**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha, wa 2014/15 Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 9.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 7.9 zilikuwa ni matumizi ya kawaida (Mishahara na matumizi mengineyo – OC) na shilingi bilioni 2.04 pekee zilkuwa ni matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kuwa na wizara inayotengewa shilinngi bilioni 9.7 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuratibu masuala ya uwekezaji. Bajeti hii ni ndogo mno na mbaya zaidi asilimia 80 ni matumizi ya kawaida na asilimia 20 tu ndio matumizi ya maendeleo ya kuwawezesha wananchi na kuratibu shughuli za uwekezaji. Haiingii akilini kwamba shilingi

bilioni 2 ndio zinatengwa kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi ambao ni zaidi ya milioni 40, na wakati mwingine fedha hizo za maendeleo hazitolewi kabisa .kwa mfano katika mwaka huu wa fedha 2014/15 serikali ilitenga kiasi cha shilingi **bilioni 1** kwa ajili ya Mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi (NECC) ambazo hadi kufikia machi, 2015 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa kabisa. Na cha kushangaza zaidi ni kwamba katika mwaka wa fedha 2015/16 Serikali imetenga kiasi hicho hicho cha fedha jambo ambalo linatia mashaka kama litatekellezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Wizara ya uwezeshaji na uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ifutwe na badala yake huduma zote zinazotolewa na Wizara hiyo zitolewe katika wizara za kisekta. Hii itapunguza ukubwa wa Serikali na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Kwa kuwa fedha nyingi zinazopelekwa katika wizara hii ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na hata zile chache zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendelleo hazitolewi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Pauline Gekul (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI**

12 Mei, 2014